

Nehemia aliposikia habari ya kwamba yerusalemu na kuta zake umebomolewa hapana aliye salia alilia na kuomba kibali kwa mfalme katika nchi aliyo kuwa akitumikia akesema moyoni mwake hatakuwa na amani kama mji wao utakuwa katika hali ya ukiwa namna hiyo **nehemia 2:4-5**. Mungu alifanya na wewe maagano katika ardhi na udongo wa kwenu na ndio maana hata ukifa leo watu wengi watataka kujua wapi ulipozaliwa ili wakauhifadhi mwili wako huko. Maana ni agizo la Mungu kwa waisraeli. Yusufu alikuwa waziri misri lakini alipo kufa mwili wake ulisafirishwa uje kuzikwa kwenye makaburi ya baba zake yaani Kwa yakobo.tena biblia inaweka wazi kwamba kunawatu baadhi yao walipokuwa wamezikwa uhamishoni mifupa yao ilifukuliwa ili wakaizike nyumbani kwao maana ni alama ya urithi. **Nehemia 2:17. Ninakuomba wewe unayesoma kitabu hiki kama haujaweka sawa mji wa nyumbani kwenu chukua hatua sasa.**